

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S. L.P 30261

Kibaha.

Simu: (023) 2402658

Nukushi: (023) 2402657

Baruapepe: [rbcpwani@pccb.go.tz](mailto:rbcpwani@pccb.go.tz)

Wavuti : [www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

TAARIFA KWA WANANCHI KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

PWANI 18 JUNE, 2020

**TAKUKURU WILAYANI RUFJI YAMSHIKILIA SALUM BAKARI MKEMI KWA  
UCHUNGUZI DHIDI YA VITENDO VYA RUSHWA KATIKA UCHAGUZI**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wilayani Rufiji mkoani Pwani inamshikilia SALUM BAKARI MKEMI mkazi wa Dar Es Salaam na mwenyeji wa wilaya ya Rufiji kwa uchunguzi kufuatia tuhuma za kujihusisha na vitendo vya Rushwa kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Viongozi uliopangwa kufanyika Oktoba 2020.

Uchunguzi wa TAKUKURU Wilaya ya Rufiji umebaini kwamba, mtuhumiwa amekuwa akidaiwa kutoa fedha na kufanya vikao na baadhi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Rufiji, na kufanya kampeni kabla ya wakati, hivyo Taasisi inamshikilia mtuhumiwa huyo kwa lengo la kufanya uchunguzi wa kina dhidi ya tuhuma hizo.

**WITO**

Nitoe wito kwa kurudia maneno ya Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU Brig.Jen. JOHN MBUNGO alipozungumza na vyombo vya habari, Juni 17, 2020 jijini Dodoma kuhusu RAI YA TAKUKURU KUELEKEA UCHAGUZI MKUU WA OKTOBA 2020 alisema “.....*dhamira ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ni kutotaka kusikia watu wakijihusisha na vitendo vya Rushwa, NA YEYOTE ATAKAYEBAINIKA ATAONJA JOTO LA JIWE LA KISHERIA*”

Aidha niwasihi sana wananchi wa Wilaya ya Rufiji na Mkoa wa Pwani kwa ujumla kukataa kurubuniwa na wachache wasio na nia njema na nchi yetu.

***KATAA RUSHWA JENGA NCHI YAKO***

Imetolewa na:

*SUZANA RAYMOND,*

*MKUU WA TAKUKURU MKOA WA PWANI*